

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 022 2112065-7
Fax No. +255 022 2112538
E-mail: info@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 9133,
DAR ES SALAAM

TAARIFA KWA UMMA

**KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE KUKUTANA DAR ES SALAAM
KUANZIA TAREHE 14 MACHI HADI 15 APRILI, 2016**

1.0 UTANGULIZI

kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati za Kudumu za Bunge zitaanza kukutana tarehe 14 Machi hadi tarehe 15 Aprili 2016 kutekeleza Majukumu yake, Jijini Dar es Salaam kabla ya Mkutano wa Bajeti wa Bunge unaotarajiwa kuanza tarehe 19 Aprili, 2016.

Hivyo, Wabunge wote wanapaswa kuwa wamewasili jijini Dar es Salaam ifikapo jumapili tarehe 13 Machi 2016 tayari kwa kuanza vikao siku ya tarehe 14 Machi, 2016.

2.0 SHUGHULI ZITAKAZOTEKELEZWA

Wakati wa vikao vya Kamati, Jukumu la Msingi katika Vikao hivyo kwa kamati zote litakuwa ni Majadiliano katika ngazi ya Kamati za Bunge na Serikali kuhusu maudhui ya Mpango wa Mwaka wa Maendeleo ya Taifa na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017. Aidha, ratiba ya Majukumu ya Kamati hizo yatatekelezwa kwa utaratibu ufuatao:

- a) Kuanzia Tarehe 14 hadi 27 Machi, 2016 Kamati zitakuwa na Vikao kwa ajili ya kujadili Taarifa mbalimbali za Serikali ambapo kila Kamati itakutana na Viongozi na Watendaji wa Serikali kutoka katika Wizara au taasisi inayoismamiwa na kamati husika.

- b) Tarehe 29 Machi, 2016 Kamati zote za Bunge zitapokea Dondoo na Randama za Vitabu vya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
- c) Siku ya Tarehe 30 Machi, 2016 Wabunge wote watapokea Mapendekezo ya Serikali kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Taifa na kiwango cha Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
- d) Kuanzia Tarehe 31 Machi hadi Tarehe 06 April 2016 Kamati ya Bajeti itachambua mapendekezo ya mpango na kiwango cha Ukomo wa Bajeti. Wakati huo huo,
- e) Kamati za Kisekta zitafanya zitatembelea na kukagua utekelezaji miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016) na Wizara au Taasisi zinazosisimamia.
- f) Baada ya kutembelea miradi ya Maendeleo, kuanzia Tarehe 07 hadi 15 Aprili 2016, Kamati zitapokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za wizara zinazosisimamia kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuchambua makadirio ya Matumizi ya serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata, 2016/2017
- g) Kamati ya Fedha na Mtambuka zitaendelea na Shughuli za uchambuzi juu ya masuala ya Fedha, UKIMWI, Bajeti na Sheria Ndogo.

3.0 SHUGHULI NYINGINE

Shughuli za Kamati zitamalizika tarehe 15 Aprili, 2016 Jijini Dar es Salaam ambapo Mkutano wa Bunge wa Bajeti utanza tarehe 19 April, 2016 Mjini Dodoma na unategemewa kumalizika kabla ya tarehe 30 Juni, 2016. Ratiba zote za Kamati zitapatikana kwenye tovuti ya Bunge ambayo ni www.parliament.go.tz

Imetolewa na:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano

Ofisi ya Bunge

Dar es Salaam

10 Machi, 2016.